**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA SERENGETI**
**SHULE YA SEKONDARI NATTA**
**S.L.P 192 Mugumu-Serengeti.**


**MAWASILIANO.**
**E-MAIL** nattasec2004@gmail.com
**M/SHULE** 0762177350/0753741530
**MAKAMU** 0759785443/0687229353
**TAALUMA** 0686777374
**MATRON** 0755057448


**Kumb. Na. NATT/F.V/JNG.VOL 1/2024** **Tarehe. 08/05/2024**

Ndugu…………………………………..
Mzazi/Mlezi wa ……………………………
S.L.P…………………….

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA MASOMO YA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI NATTA MWAKA 2024.**

Ninayo furaha kukujulisha kuwa mwanao …………………………………………….amechaguliwa kujiunga na masomo ya Kidato cha **TANO** tahasusi ya ……………… katika shule ya sekondari NATTA ambapo atapata Elimu na hatimaye kulitumikia Taifa. Kama Mzazi/Mlezi unapaswa kumuasa mwanao azingatie masomo pamoja na taratibu zote za shule na kumpa mahitaji yote ya shule ili aweze kulifikia lengo hili la Kitaifa. Aidha, aelewe kuwa ni miongoni mwa Watanzania wachache waliopata nafasi hii adhimu na anapaswa kuitumia vyema.

Shule ya Sekondari Natta iko katika Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti Mkoani Mara, umbali wa Kilomita 40 kutoka Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya-Mugumu. Usafiri wa barabarani ni wa uhakika muda wote.

Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe 01/07/2024 Mwanao anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 08/07/2024 Muda wa kuripoti ni kuanzia **saa 2:00 asubuhi hadi saa 11:00 Jioni siku za kazi Tu**. Mwanafunzi anatakiwa kuwa ameripoti shuleni si zaidi ya **wiki mbili (siku 14)** tangu tarehe ya muhula wa kwanza kuanza. Mara mwanafunzi afikapo shuleni **aripoti Ofisi ya Makamu Mkuu wa Shule kwa ajili ya mapokezi na Usajili.**

Pia mwanafunzi ajapo shuleni ni muhimu aje na vitu vifuatavyo;

i. **Mahitaji yote yaliyoelekezwa katika fomu hii**
ii. Fomu iliyojazwa na Daktari katika hospitali ya SERIKALI kuhusu Afya ya Mwanafunzi (Medical Examination Form).
iii. Fomu iliyojazwa ya maelezo binafsi ya mwanafunzi (Personal Particularas Form).

iv. Fomu ya kukubali masharti ya shule. Wewe na mwanao muisome kwa kina pamoja na sheria za shule mkizikubali, msaini fomu hizo na ziwasilishwe shuleni hapa wakati wa kuripoti.

**v. Aje na Ream ya karatasi (Double A) Zinatakiwa 2 kwa mwaka.**

vi. FOMU ya usajili wa mzazi/mlezi/ndugu wa karibu wa mwanafunzi.

**ZINGATIA: HATUPOKEI MWANAFUNZI SIKU NA SAA AMBAZO SIYO ZA KAZI.**

…………………………….

**MKUU WA SHULE**

## JINSI YA KUFIKA SHULENI

**i.** Kwa wanaotokea Dar Es Salaam, Pwani, Morogoro, Mikoa ya Kati, Kusini, Nyanda za juu Kusini, Kigoma na Kagera; baada ya kufika Mwanza wanashauriwa kupanda mabasi stendi ya NYAMHONGORO-MWANZA yanayoelekea MUGUMU kupitia BUNDA. Nauli kutoka MWANZA hadi NATTA ni kati ya Tsh. 10,000/= hadi Tsh. 12,000/=.

**ii.** Kwa wale wanaotokea Mikoa ya Kaskazini (Kilimanjaro, Arusha, Manyara na Tanga) wapande mabasi yanayokwenda MUSOMA kupitia barabara ya NGORONGORO- SERENGETI. Nauli kutoka ARUSHA Mjini hadi NATTA ni Tsh. 45,000/=

**iii.** Kwa wale wanaotoka Mkoa wa MARA (Musoma MC, Musoma DC, Tarime, Ryorya, Bunda Mji, Bunda V na Butiama) wanaweza kupandia magari kutoka katika Stendi kuu za Mabasi zilizoko maeneo yao kuelekea NATTA-MUGUMU kupitia Bunda, Musoma, Tarime au Butiama kupitia Isenye na Kushukia NATTA Sekondari. Nauli ni kati ya Tsh. 10,000/= hadi Tsh. 15,000/= kufika shuleni.

**KUMBUKA**

Mwanafunzi anapaswa/anashauriwa kumwambia/kumkumbusha Mhudumu wa Gari (Dereva au Kondakta) wa Gari alilopanda ili amshushe **NATTA SEKONDARI (SHULE IPO BARABARANI)**.

**OFISI YA RAISI, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA SERENGETI**
**SHULE YA SEKONDARI YA NATTA**

**ORODHA KAMILI YA MAHITAJI YA LAZIMA KWA KILA MWANAFUNZI**

**MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.**

**2.1 Ada na Michango ya Shule:**

**Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi ni:-**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**JUMLA YA MICHANGO YOTE NI TSH. 80,000/=.**

Fedha hiyo ilipwe katika akaunti ya Shule Na. **30201200045 iitwayo NATTA SECONDARY SCHOOL katika Benki ya NMB Tawi lolote na alete Bank Pay in Slip Original Shuleni iliyo andikwa Jina sahihi la Mwanafunzi.**

**2.2. Sare ya Darasani:**

(i) Sketi mbili (2) za Dark Blue. Kwa mzazi atakayependa kununua shuleni zinapatikana kwa gharama ya Tsh 40000/= kila moja Tsh 20000/=. Mshono ni Linda Box. Sketi iwe ndefu hadi usawa wa kifundo cha mguu.
(ii) Shati (blouse) mbili (2) nyeupe za mikono mirefu na isiyobana mwilini.
(iii) Viatu vyeusi vya Ngozi vya kufunga kwa Kamba vyenye visigino vifupi jozi 2

(iv) Sweta moja (1) nzito la Dark Blue yenye V shingoni. Kwa mzazi atakayependa kununua shuleni linapatikana kwa gharama ya Tsh 12000/= (Rangi ya Dark Blue).

(v) Wanafunzi wenye Imani ya kiislamu **wataruhusiwa kushona hijabu inayofanana na sare ya shule** (Iwe ya rangi nyeupe isiyo na urembo) jozi mbili (2).

(vi) Soksi nyeupe ndefu jozi mbili (2)

N.B: NI MARUFUKU MWANAFUNZI KUSUKA NYWELE KWA MTINDO WOWOTE ULE, KUWEKA DAWA (BLICH) KICHWANI, KUTUMIA VIPODOZI VIKALI VINAVYOWEZA KUATHIRI NGOZI YAKE AU KUJA NA NGUO YOYOTE YA NYUMBANI.

**2.3 VIFAA VYA KUTUMIA DARASANI NA WAKATI WA MITIHANI**

1. Mathematical set kwa wanaochukua Geography
2. Non Programable Calculator kwa wanaochukua GEOGRAPHY
3. Kamusi (English Dictionary) kwa wanaochukua masomo ya LUGHA
4. Madaftari makubwa yasiyopungua 9 kwa ajili ya nukuu za masomo na Madaftari mengine 9 kwa ajili ya mazoezi ya darasani.
5. Kalam na penseli
6. Ream moja (Double A) kila muhula kwa ajili ya mitihani na majaribio.Ream isiyo Double A haitapokelewa.
7. Aje na vitabu vya masomo angalau matatu ili kupunguza uhaba wa vitabu shuleni **(ni mali ya mwanafunzi**)
8. Begi la mgongoni la kubebea daftari na vifaa vya kusomea.

9. File moja kwa ajili ya kuhifadhi nyaraka muhimu na kumbukumbu za maendeleo ya mwanafunzi.

## 2.4 MAHITAJI YA BWENI

- Sanduku la chuma la kutunzia vifaa vyake binafsi na kufuri imara.
- Njoo na godoro la futi 2.5x6.
- Shuka mbili rangi ya pink, blanketi rangi yoyote, mto na foronya rangi ya pink.
- Galoni ya lita 5 ya kuhifadhia maji ya kunywa.
- Neti ya mbu futi 4x6 (rangi nyeupe)
- Gauni la kushindia (shamba dress) Kitambaa kizito namba moja, rangi ya kijivu Mshono SOLO. Kwa mzazi atakayependa kununua shuleni linapatikana kwa gharama ya tsh 20000/=.
- Sketi moja ya kushindia inapatikana shuleni kwa mzazi atakayependa kununua shuleni kwa gharama ya Tsh. 20000/= (kitambaa rangi ya ORANGE-mshono LINDA BOX YENYE MIKANDA YA BEGANI-UREFU UNAOZIDI MAGOTI)
- Tracksuit nzito moja rangi ya DARK BLUE yenye ufito mweupe pembeni. Pia, inapatikana shuleni kwa mzazi atakayependa kununua shuleni kwa gharama ya tsh 25000/=.
- Tshirt 2 zenye nembo ya shule. Kwa mzazi atakayependa kununua shuleni zinapatikana kwa gharama ya Tsh 25000/=
- Toilet tissue za kutosheleza matumizi yake.(Zinapatikana katika duka la shule)
- Pedi za kutosha (zinapatikana katika duka la shule)
- Kiwi nyeusi na brush yake.
- Vifaa vya usafi {**SOFT BLOOM 1 na Jembe 1**}.
- Tochi aina ya D.Light moja kwa matumizi wakati umeme unapokatika.
- Malapa/kandambili za kuendea bafuni.
- Kanga/kitenge jozi moja,taulo moja na nyuzi za kuogea.
- Mafuta ya kujipaka mwilini, sabuni,miswaki na dawa ya meno.
- Saa ya kuvaa mkononi.
- Fedha ya matumizi binafsi ya mwanafunzi isiyopungua Tsh 40,000/=

**NB:Baadhi ya uniform zitapatikana shuleni kutokana na ushauri wa wazazi/walezi.**

## 2.5. Huduma ya chakula shuleni.

Njoo na vifaa vya chakula (sahani, kikombe, na kijiko). Mwanafunzi atakula chakula kilichoandaliwa shuleni.

## 2.6. Gharama za matibabu

Jukumu la matibabu ni la mzazi/mlezi wa mwanafunzi. Shule itahusika na huduma ya kwanza tu. Endapo mwanafunzi ana magonjwa ya kudumu mfano Pumu (Asthma) anashauriwa kuja na dawa anazotumia au bima ya afya kama anayo. TUNASISITIZA MWANAFUNZI KUWA NA KADI YA BIMA YA AFYA. **Kwa wanafunzi ambao hawana bima waje na pesa kiasi cha Tsh 50400/= kwa ajili ya kukatia Bima mhimu sana.**

**3.0: SHERI NA KANUNI ZA SHULE.**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya Elimu, Sayansi, na Teknolojia nchini chini ya ofisi ya Rais -TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala mara baada ya kuripoti shuleni.

1. Heshima kwa watu wote (viongozi wa serikali, madhehebu ya dini, vyama vya siasa, viongozi wa serikali ya wanafunzi,walimu, wanafunzi wengine Pamoja na wazazi)
2. Mahudhurio mazuri katika shughuli za ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
3. **Kusaini mkataba maalum wa taaluma shuleni kuhusu kufanya vizuri na kufaulu mitihani.**
4. Kushiriki kwa makini katika kufanya maandalio ya jioni.
5. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine zitakazo tolewa.
6. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
7. Kutunza usafi wa mwili, mavazi, na mazingira ya shule.
8. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
9. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
10. Kutunza mali za umma.

**3.1: Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha ukafukuzwa au kusimamishwa shule:**

1. Wizi wa mali ya shule na wanafunzi wengine.
2. Kujihusisha na ngono, uasherati, ushoga, ulawiti, usagaji na ubakaji.
3. Ulevi wa pombe na kujihusisha na madawa ya kulevya.
4. Kupiga, kupigana na kuchochea ugomvi.
5. Kuharibu mali ya umma kwa makusudi na kukataa kulipa fidia ya uharibifu.
6. Kukataa kupokea adhabu halali na kuonyesha kiburi,dharau na ufedhuri.
7. **Mwanafunzi kumiliki au kutumia au kukutwa na simu au "line" katika mazingira ya Shule.**
8. Kuolewa, kupatikana na ujauzito, kutoa mimba au kushawishi kutoa mimba.
9. Kushiriki au kushawishi kugoma, kuchochea au kuvuruga amani na usalama wa shule na watu wengine.
10. Kudharau bendera ya Taifa,viongozi wa serikali, vyama vya siasa, madhehebu ya dini na viongozi wa shule.
11. Utoro wa muda mrefu, kushindwa kufanya kazi za darasani na nje.
12. Kushindwa kufanya mazoezi/majaribio/mitihani kwa makusudi Pamoja na kutohudhuria maandalizi ya usiku (night preparation).
13. Kutoa lugha ya matusi kwa walimu, wafanyakazi wasio walimu na viranja.
14. Kulala nje ,kutembelea majumba ya starehe na nyumaba za kulala wageni.
15. Kutumia vifaa vya umeme kama vile heater,radio na pasi ya umeme.
16. **Kutembelea nyumba za walimu/watumishi wa shule kwa namna yoyote ile**.
17. Kujipikia/kuingiza vyakula au kileo chochote bwenini.
18. Kukutwa nje ya shule bila ruhusa na mavazi yasiyoruhusiwa shuleni.
19. Kudharau bendera ya Taifa, wimbo wa Taifa na viongozi wa Nchi.
20. Kufanya jaribio lolote la kujiua, kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k
21. Kusuka nywele au kunyoa mtindo wa kihuni.

**4.0: Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi:**

i. Fomu ya hospitali (medical examination form) ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara mwanafunzi atakaporipoti shuleni.

ii. Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo, makosa ya jinai.

iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni, na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

iv. Barua/fomu ya kukuita shuleni.

**5.0: Hitimisho muhimu**

Tafadhali soma kwa umakini maelezo haya na kuyatekeleza kikamilifu

1. Hatupokei fedha taslimu shuleni. Hivyo malipo yote yapitie **BENKI** isipokuwa malipo ya vifaa vinavyoweza kupatikana shuleni.

2. Mwanao haruhusiwi kuja shuleni na simu ya kiganjani, pasi ya umeme, redio, heater, computer na TV. AKIPATIKANA NA VIFAA HIVI, ADHABU NI KUONDOLEWA SHULENI PAMOJA NA KULIPA FIDIA YA UHARIBIFU WA MIUNDOMBINU YA SHULE KIASI KISICHOPUNGUA TSH. 350,000/=

3. Haturuhusu mwanafunzi kutembelewa shuleni na watu wasio fahamika.

4. Mwanafunzi anatakiwa kuwahi bwaloni mara kengele ya chakula inapogonga akiwa na vyombo vya chakula.

5. Shule haina utaratibu wa kutoa chakula maalum (special diet) kwa wale wenye matatizo ya kiafya ya kutokula baadhi ya vyakula.

6. Mwanafunzi atumiwe nauli mapema kabla ya kufunga shule ili utaratibu wa usafiri uweze kuandaliwa mapema.

7. Ratiba ya shule huanza saa 11:30 Alfajiri kwa mchakamchaka, kufanya usafi binafsi na usafi wa mazingira ya bwenini.

8. Mwanfunzi ataruhusiwa kusali katika dhehebu lake shuleni kulingana na utaratibu uliowekwa na shule.

9. Mawasiliano ya mwanfunzi na mzazi/mlezi yapitie katika uongozi wa shule. HATURUHUSU MWANAFUNZI KUPIGA SIMU SHULENI, BALI ATATUMIA UTARATIBU WA MAWASILIANO ULIOWEKWA NA SHULE.

Hakikisha mwanao anakuja na mahitaji yote muhimu na anaripoti kwa wakati akiwa na;

- Barua/Fomu hii ya kujiunga shuleni.
- Bank pay slip original ya malipo ya kulipia benki.
- Nakala ya Result Slip inayoonyesha matokeo ya kidato cha IV.
- Nakala ya cheti cha kuzaliwa kama anacho.
- Fedha ya kulipia mahitaji yanayopatikana shuleni kama ilivyoelekezwa kwenye fomu.
- Vifaa/mahitaji yote muhimu kwa matumizi binafsi/shule.
- Fomu ya hospitali na maelezo binafsi zijazwe kwa usahihi.

**SCHOOL MOTTO: "STRIVE FOR EXCELLENCY"**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI NATTA.**

**FOMU YA KUKIRI KUKUBALIANA NA TARATIBU ZA SHULE**

**SEHEMU YA I: IJAZWE NA MWANAFUNZI MWENYEWE**

Mimi………………………………………………………………. Nimezisoma **sheria ,kanuni na taratibu za shule** na kuzielewa vizuri bila ya shaka yoyote. Ninaahidi kuzitii na kutozivunja katika kipindi changu chote cha kusoma kwangu katika shule ya Natta sekondari. Vilevile, nitajitahidi kusoma kwa bidi na kushiriki shughuli zote za nje kulingana na ratiba ya shule. Endapo nitakwenda kinyume na kiapo cha ahadi yangu, basi uongozi wa shule unichukulie hatua za kinidhamu ikiwa ni Pamoja na **kupewa adhabu kali/kusimamishwa masomo na hata kufukuzwa shule.**

**Dini……………………………Dhehebu……………………………Tarehe ya kuzaliwa………………..**

**Michezo uipendayo/Hobbies…………………………………………………………………………...**

**Kazi ya mzazi/mlezi……………………………………………mahali……………………………………….**

**Wilaya…………………………………….Mkoa…………………………Simu…………………………**

**Jina la mwanafunzi…………………………………………..Sahihi……………………Tarehe……….**

**SEHEMU YA II: IJAZWE NA MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI**

Mimi……………………………………………………………………ambaye ni mzazi/mlezi wa mwanafunzi…………………………………………………………... kidato cha tano mwaka 2021;

Ninakiri kuwa nimeyasoma maelekezo ya kujiunga na shule ya sekondari Natta na kuyaelewa vizuri. **Ninaahidi** kushirikiana na uongozi wa shule katika kuhakikisha mwanangu anazingatia taratibu zote za shule wakati wa kipindi chote cha masomo yake. Pia, **nitampatia** mahitaji yake yote muhimu ya shule ikiwa ni Pamoja na malipo, mahitaji binafsi na kufuatilia mwenendo wake kitaaluma na nidhamu na **niko tayari** kupokea maamuzi yoyote yatakayotolewa na uongozi wa shule endapo mwanangu atavunja taratibu, kanuni na sheria za shule.

Mwisho, endapo nitashindwa kutimiza jukumu langu la kumlipia mwanangu ad ana michango halali ya shule kwa wakati, niko tayari kuwajibishwa ikiwa ni Pamoja na kufikishwa katika vyombo vya kisheria kwani kufanya hivyo ni kuzorotesha maendeleo ya mwanangu na mipango ya shule kwa ujumla.

**Jina la mzazi/mlezi………………………………………………Sahihi…………………Tarehe……......**

**SEHEMU YA III: UHUSIANO WA MWANAFUNZI NA NDUGU/JAMAA WENGINE.**

Tafadhali jaza majina, namba za sim una kuonyesha uhusiano uliopo kati ya ndugu/jamaa wa mwanafunzi kwa ajili ya kurahisisha mawasiliano na uongozo wa shule.

| NA | JINA LA NDUGU | UHUSIANO | NA. SIMU | ANAKOISHI | KAZI |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |

**ASANTE KWA USHIRIKIANO**

**SHULE YA SEKONDARI NATTA**

**FOMU YA KUTHIBITISHA AFYA YA MWANAFUNZI**

(Ijazwe na mganga wa hospitali ya serikali au kituo cha afya cha serikali tu)

Kumb. Na. KSS/MEDICAL/ F.V Tarehe………………….

Mganga Hospitali/ Kituo cha Afya……………………………………

S.L.P…………………………..

………………………………….

**YAH: KUPIMWA HALI YA AFYA YA MWANAFUNZI**…………………………………….

Shule ya sekondari Natta inakuomba kupima na kujaza taarifa ya Afya ya mwanafunzi mtajwa hapo juu kabla ya kujiunga na masomo asekondari.

i. Macho (vision)…………………………………………………………………………

ii. Kifua kikuu (TB)………………………………………………………………………

iii. Pumu (Asthma)……………………………………………………………………..

iv. Shinikizo la damu(BP)…………………………………………………………..

v. Kisukari(Diabetes)……………………………………………………………………

vi. Magonjwa ya zinaa(Veneral diseases)……………………………………………..

vii. Matatizo ya usikivu……………………………………………………………

viii. Malaria sugu……………………………………………………………………….

ix. Ulemavu wa viungo(Physical disability),Taja…………………………………….

x. Mimba..........................................................................................................................

xi. Matatizo ya akili(Mental disability)……………………………………………….

xii. Matatizo ya moyo…………………………………………………………………….

xiii. Matatizo ya tumbo…………………………………………………………………

xiv. Damu(Blood examination)…………………………………………………...

xv. Kusumbuliwa na kichwa (Headache)…………………………………………...

xvi. Kichocho...................................................................................................................

xvii. Maradhi mengine…………………………………………………………...

NB: Endapo kuna maradhi yamebainika mwanafunzi apatiwe matibabu kabla ya kuja shuleni.

Nimemfanyia vipimo mwanafunzi tajwa hapo juu, Ninathibitisha kwamba afya yake ni njema/si njema kuendelea na masomo ya kidato cha tano.

**Jina la mpimaji………………………………………………………………………………**

**Sahihi…………………………………………………………………………………………**

**Cheo………………………………………………Kituo………………………Tarehe…………………...**

**ORODHA YA VITABU**

| NA | IDARA | VITABU |
|---|---|---|
| 1. | HISTORY | 1. Advanced level history paper one & two by Zisti Kamili.<br>2. Understanding African history. Advanced level paper one by Joannes Biginuamungu & George Tumani.<br>3. Mastering advanced level history book One & Two (2010) by Kato, A.<br>4. Contemporary history events. paper 1 &2 BY Shibitali C.K<br>5. History from 5&6 by Scsu & MoEVT-Zanzibar |
| 2. | GEOGRAPHY | 1. A practical Guide to statistical Maps and Digrams by<br>H.C.Truman<br>2. Practical geography for Africa by J.M.Pritchard<br>3. Principle of physical geography by F.J.Monkhouse 4. Human and economic geography by D.T. Msabila<br>5. Map reading by Zisti Kamili.<br>6. Photo interpretation by Kura<br>7. Physical geography A-Level by D.T Msabila<br>8. Physical geography by R.Bunnet<br>9. Introducing physical geography and map reading by Simon Ross |
| 3. | ENGLISH LANGUAGE | 1. Advanced literature by Nyambari Nyangwine<br>2. The real English Advanced level by Dr. Michael Kadeghe.<br>3. New advanced level English by Charles E. Shalua<br>4. Introduction of phonology by Gimson<br>5. A University grammar of English<br>6. A complete English course for form V & VI by Dr. Michael Kadeghe<br>7. Oxford advanced learners dictionary |